Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la "Manifestations of Allah" kilicho andikwa na Ab Muhammad Zaynu'l 'bidin.

Kitabu hiki ni ufafanuzi wa du'a mashuhuri inayosomwa katika Mwezi mtukufu wa Ramadhani. Mwandishi ameeleza kwa ufasaha kabisa kwamba, ili du'a iwe ni yenye kukubaliwa lazima iambatane na vitendo vya mtu kuhusiana na du'a anayoimba. Kwa mfano katika du'a hii tunamuomba Allah swt: "Ewe Allah ingiza furaha kwenye roho za wakazi wa makaburini," lakini kama wewe hujishughulishi kwenda kuzuru makaburi kama alivyosisitiza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wala huwatolei maiti wako sadaka pamoja na kwamba uwezo unao wa kufanya hivyo, ni muhali du'a yako hiyo kukubaliwa. Au kama tunavyoomba katika du'a hii kwamba Allah swt, amtajirishe kila aliye fukara, amshibishe kila mwenye njaa, amvishe kila ambaye hana nguo n.k. Lakini sisi tukawa hatujishughulishi kuwasaidia wenye shida kama hizo, basi itakuwa kama kumkejeli Mwenyezi Mungu.

Katika kufafanua vipengele vya du'a hii, mwandishi amejitahidi sana kuwazindua watu na kuwa hamasisha ili waone umuhimu wa du'a na utekelezaji wake ili iwe yenye maana na manufaa kwa mwenye kuomba na mwenye kuombewa.

Kutokana na umuhimu wa du'a hii tumeona tukitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa lengo letu lile lile la kuwahudumia ndungu zetu Waislamu wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru Ndugu yetu Dr. M. S. Kanju kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vile vile tunawashukuru wale wote walioshiriki katika kusahihisha na kukipitia hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu katika dini.

Mchapishaji:
Tabligh Sub committee
KSI Jamaat – Daressalaam

P O Box 233, Daressalaam. Tanzania. Tel – 255 22 2115119

Fax – 255 22 2113107

Email tabligh@raha.com [1]

Website: www.tabligh.org [2]

Source URL: https://www.al-islam.org/fr/node/39623#comment-0

Links

[1] mailto:tabligh@raha.com

[2] http://www.tabligh.org